

# Ni Mtakatifu Bwana Mungu wetu

Zaburi 137, 1-2a, 2bc-3, 4-5, 7c-8

Siku ya Mungu ya tano katika mwaka C

Eugène AMPIRE

♩ = 100

S  
A

Ni Mta - ka - ti - fu Bwa - na Mu - ngu we - tu.

T  
B

7

1. Nitakutukuza, ee Bwana, kwa moyo wangu wote,  
Kwani umesikia maneno ya kinywa **changu**.  
Mbele ya malaika nitakuimbia,  
Nitaliangukia hekalu lako takatifu.
2. Nitatukuza jina **lako**,  
Kwa ajili ya wema na uaminifu **wako**.  
Siku nilipokuita ulinisikiliza,  
Uliongeza nguvu rohoni **mwangu**.
3. Wafalme wote wa dunia watakutukuza, ee Bwana,  
Watakaposikia maneno ya kinywa **chako**.  
Wataziimbia njia za Bwana:  
Kweli, utukufu wa Bwana ni **mkubwa**.
4. Mkono wako wa kuume unanisalimisha;  
Bwana atatimiliza kwangu aliyonitenda.  
Ee Bwana, wema wako ndio wa milele:  
Usiache kazi ya mikono **yako**.